

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA KATIBA NA SHERIA**

**Telegramu: "LEGAL"**  
**Simu Na.: +255 26 2310019**  
**Nukushi: +255 26 2310056**  
**Barua Pepe: km@sheria.go.tz**  
**DodomaTovuti:[www.sheria.go.tz](http://www.sheria.go.tz)**



Mji wa Serikali Mtumba,  
Mtaa wa Katiba,  
S. L. P. 315,  
**40484 DODOMA**

**TAARIFA KWA UMMA  
KULAANI KITENDO CHA UDHALILISHAJI NA UKATILI  
WA KIJINSIA**

*Dodoma, 05 Agosti, 2024.*

Kuna video iliyosambaa kwenye mitandao ya kijamii ikimuonyesha mwanamke anayesemekana anatoka eneo la Yombo Dovya Jijini Dar es Salaam akifanyiwa vitendo vya udhalilishaji kinyume na sheria na maadili ya nchi.

Wizara ya Katiba na Sheria inaungana na Jeshi la Polisi na kuwasih raia wema kutoa taarifa kuhusu tukio hili kwa jeshi hilo. Kila binadamu anastahili heshima, haki na usawa katika jamii yetu. Tunatoa wito kwa jamii kusimama pamoja kupinga unyanyasaji na udhalilishaji wa kijinsia.

Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zake zinazohusika na masuala ya haki zinaendelea kufuatilia suala hili kwa karibu ili sheria ichukuwe mkondo wake na haki itendeke. Tanzania bila ukatili wa kijinsia inawezekana.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read "Mwakabuku".

Lusajo Mwakabuku

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

**Wizara ya Katiba na Sheria**